



# Sherehe ya Sandra



Tusome Early Literacy Programme

# Sherehe ya Sandra



Jumamosi ilikuwa tarehe ya kuzaliwa kwa Sandra.

Sandra alifurahi kwa sababu alitarajia zawadi kutoka kwa jamaa na rafiki zake.





Sandra alienda na mama yake sokoni kununua vitu vya sherehe.


Kwanza waliingia dukani wakanunua keki,  
peremende na biskuti.





Baadaye walielekea sokoni kununua matunda, nyama, nyanya, vitunguu na sukumawiki.

Sandra alimkumbusha mama yake anunue soda na gololi pia.





Walirudi dukani wakanunua soda lakini hawakununua gololi kwa sababu pesa ziliisha.



Walipomaliza, walirudi nyumbani kusherehekea kuzaliwa kwa Sandra.

## Maswali

1. Sherehe ya kuzaliwa kwa Sandra ilikuwa siku gani?
2. Kwa nini Sandra alifurahi?
3. Sandra na mama yake walinunua nini dukani?
4. Sandra na mama yake walinunua nini sokoni?
5. Kwa nini Sandra na mama yake hawakununua gololi?

# Sherehe ya Sandra

Ni siku muhimu kwa maisha ya Sandra. Anasherehekea kuzaliwa kwake. Sandra anamfuata mama yake sokoni kununua bidhaa za sherehe. Je, Sandra atapata kila kitu atakachotaka sokoni?



Kitabu hiki kimechapishwa kwa ufadhili kutoka kwa Shirika la maendeleo ya kimataifa la Marekani (USAID/Kenya) na Idara ya maendeleo ya kimataifa ya Uingereza (DFID/Kenya) kupitia mradi wa Tusome Early Grade Reading Activity.